



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

(Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: 023-2510013, 2510031
Nukushi: +023-2510031
Baruapepe: ded@masasidc.go.tz
Tovuti: <http://www.masasidc.go.tz>

S.L.P.60
Masasi
Mtwarra
TANZANIA

Unapojibu tafadhalii taja:

Kumb. Na.MDC/L.10/2/VOLX/4

Tarehe: 03/02/2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi anapenda kuwatangazia watanzania wote wenye sifa zilizoorodheshwa kwenye tangazo hili kujaza nafasi moja(1) ya ajira ya kudumu ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III. Ajira hiyo imetokana na kibali cha **Ajira Mbadala** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora chenye Kumb.Na FA.170/362/01 "B"/29 cha tarehe **21/12/2021**.

1. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 1)

1.1: KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III

- Atakuwa mtendaji na mshauri mkuu wa serikali ya kijiki na kamati zake katika kupanga mipango ya maendeleo na utekelezaji wake.
- Atakuwa Afisa Masuuli wa serikali ya kijiki na atasimamia mapato na matumizi ya serikali ya kijiki.
- Ataratibu na kusimamia na upangaji na utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kijiki.

- Atakuwa mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika kijiji.
- Atakuwa katibu wa serikali ya kijiji.
- Atatafsiri sera,taratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo za kijiji.
- Ataratibu na kuandaa taarifa ya utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuziwasilisha kwenye halmashauri ya kijiji na baadaye kwenye mukutano mkuu wa kijiji.
- Ataratibu vikao vya maendeleo ya kijiji vitakavyohusisha wananchi na wataalamu waliopo kwenye eneo lake.
- Atasaidia katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa,umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Atasimamia na kuratibu matumizi bora ya nguvu kazi.
- Atakuwa kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalamu katika kijiji.
- Atasimamia ukusanyaji wa kumbukumbu za walipa kodi,wataalamu mbalimbali wa NGOs zilizopo katika kijiji.

1.2: SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu kidato cha nne au sita na mafunzo ya astashahada/cheti katika moja ya fani zifuatazo:Utawala,Sheria, elimu ya jamii, usimamizi wa fedha, maendeleo ya jamii na sayansi ya jamii kutoka chuo chochote kinachotambulika na serikali.

1.3:NGAZI YA MSHAHARA

Kwa kuzingatia ngazi ya mshahara ya serikali TGS B₁

1.4: MASHARTI KWA UJUMLA

i/ Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.

ii/Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.

iii/ Waombaji waambatanishe maelezo binafsi(CV) yenyenye anuani na namba zao za simu na majina mawili ya wadhamini.

iv/Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma na kuhitimu mafunzo ya vyuo.

v/ Maombi yaambatanishwe na picha (**passport size**) ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma.

vi/ Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatanishe cheti cha ulinganifu (Equivalent Certificates) kutoka Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) au kwenye mamlaka husika.

vii/ Mwombaji mwenye vyeti vya ngazi ya **NTA Level 4 (Basic Technician Certificate)** maombi yao hayatafanyiwa kazi. Cheti kinachopokelewa ni (**Technician Certificate NTA Level 5** au **(Certificate)**).

viii/ Watakaochaguliwa kufanya usaili watajulishwa tarehe ya usaili kupitia tovuti ya Halmashauri www.masasidc.go.tz

ix/Maombi yatapolewa kuanzia tarehe **04/02/2022** Hadi tarehe **17/02/2022**.

x/Mwombaji wa nafasi ya kazi awe na namba ya Utambulisho wa Taifa(NIN) Kutoka NIDA.

x/Maombi yatumwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa anuani ifuatayo:

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI

S.L.P 60

MASASI

Tangazo hili limetolewa na;



JOSHUA E. SANGA
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)

MASASI

MKURUGENZI MTENDAJI

HALMASHAURI YA WILAYA

S. L. P. 60³, MASASI